



RIPOTI YA KIHAIIDROLOJIA JARIDA LA MWEZI

BWAWA JULIUS NYERERE (JNHPP)

JULAI, 2026

Tarehe ya Utekelezaji: 24 Nov 2025
Toleo, No: 00



"KILA TONE LINATHAMANI"

Tarehe ya Utekelezaji: 24 Nov 2025
Toleo, No: 00


Muhtasari wa Hali ya Maji

Kituo cha Kufua Umeme cha Julius Nyerere (JNHPP) kipo katika Bonde la Stiegler kwenye Mto Rufiji, nchini Tanzania. Kituo hiki hupokea maji kutoka katika mito mikuu mitatu ya Bonde la Rufiji, ambayo ni Mto Great Ruaha, Mto Kilombero na Mto Luwegu. Mito hii kwa pamoja huchangia maji yanayohitajika kwa uzalishaji wa umeme.

Mbali na uzalishaji wa umeme, mito hii ina mchango mkubwa katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa kuwezesha shughuli za kilimo, upatikanaji wa maji kwa matumizi ya majumbani na viwandani, ufugaji, pamoja na kuhifadhi uwiano wa mifumo ya ikolojia ndani ya Bonde la Rufiji..

Hadi mwishoni mwa Julai 2026, hali ya wingi wa maji katika mito inayoingiza maji katika bwawa la JNHPP ulikuwa juu ya wastani kwa asilimia 141 ukilinganishwa na wastani wa muda mrefu wa mwezi husika. Hali hii ilichangiwa na mvua zilizonyesha kwa kiwango cha wastani katika maeneo ya juu ya vyanzo vya mito pamoja na usimamizi mzuri wa rasilimali za maji katika Bonde la Rufiji.

Kutokana na hali hiyo, kiwango cha maji katika bwawa la Kituo cha Kufua Umeme cha Julius Nyerere kilifikia mita 183.43 juu ya usawa wa wastani wa bahari (amsl) tarehe 31 Julai 2026, sawa na asilimia 101.91 ya wastani wa muda mrefu wa mwezi Julai.



Hali ya Hewa

Hali ya Mvua – Julai 2026:

Takwimu za mvua zinaonesha kuwa maeneo mengi ya Bonde yalikuwa na hali ya ukavu katika kipindi chote cha Julai 2026. Kutokana na hali hiyo, maji yaliyotiririka juu ya uso wa ardhi yalikuwa machache, hivyo kusababisha kupungua kwa mtiririko wa maji katika mito na vijito, hususan vile vinavyotegemea mvua za msimu.


Mwelekeo wa Hali ya Hewa – Agosti 2026:

Kwa mujibu wa utabiri wa hali ya hewa uliotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA):


Maeneo mengi ya Bonde la Rufiji yanatarajiwa kuendelea kuwa na hali ya ukavu katika kipindi chote cha Agosti 2026.

Wiki ya Kwanza	Wiki ya Pili	Wiki ya Tatu	Wiki ya Nne
Halia ya ukavu kwa ujumla	Halia ya ukavu kwa ujumla	Halia ya ukavu kwa ujumla	Halia ya ukavu kwa ujumla


Utabiri wa Mvua
Wiki 01 Agosti, 2026




Utabiri wa Mvua
Wiki 02 Agosti, 2026



Utabiri wa Mvua
Wiki 03 Agosti, 2026



Utabiri wa Mvua
Wiki 04 Agosti, 2026




Hali ya Mtiririko wa Maji

Vituo vya Kihaidrolojia

Wastani wa mtiririko wa maji katika mito inayoingia JNHPP kwa mwezi Julai 2026 uliendelea kuwa juu ya wastani wa muda mrefu (LTA: 2000–2025). Jedwali la 1 linaonesha ulinganisho wa wastani wa mtiririko wa maji uliorekodiwa mwezi Julai 2026 na wastani wa muda mrefu kwa kipindi hicho.


Matokeo ya Kihidrolojia

Hali ya wingi wa maji yanayoingia katika Bwawa la Julius Nyerere imeonyesha kupungua katika kipindi cha Julai kuelekea Agosti. Hata hivyo, usawa na kiwango cha maji katika bwawa kiliendelea kubaki juu ya wastani wa muda mrefu, hali inayoonyesha uwepo wa mtiririko thabiti wa maji katika mito.



Jedwali 1: Mchanganuo wa Takwimu za Wingi wa Maji (Julai, 2026)

Na	Namba ya Kituo	Mto	Wastani Wingi Julai 2026 (m³/s)	Wastani Wingi wa Maji LTA Julai 2000–2025 (m³/s)	Maelezo
1	1KA3B	Great Ruaha at Msolwa	117	67.51	Juu zaidi ya Wastani
2	1KB17A	Kilombero at Swero	281.29	176.52	Juu zaidi ya Wastani
3	1KC3A	Luwegu at Mbarang'andu	9.64	10.8	Wastani




Hali ya Maji Bwawani

Kufikia mwisho wa mwezi Julai 2026;

kiwango na usawa wa maji katika bwawa umeendelea kuwa juu ya ukilinganisha na wastani wa muda mrefu. Hali hii imechangiwa mvua zilizokuwa za wastani na juu ya wastani zilizonyesha wakati wa msimu wa masika pamoja na usimamizi endelevu wa rasilimali za maji katika Bonde.

Uchambuzi

Usawa wa maji katika bwawa la JNHPP ulifika mita183.43 juu ya usawa wa bahari sawa na asilimia 101.91 ukilinganisha na wastani wa muda mrefu kwa mwezi husika. Hali hii inaonesha kuwa maji yaliyohifadhiwa katika bwawa yanatosheleza mahitaji ya uzalishaji wa umeme, hivyo kuwezesha kituo kuendelea kuzalisha umeme kwa uwezo wake kamili kwa kutumia nguvu ya maji.



Mapendekezo

- Inapendekezwa mabwawa yaendeleo kuendeshwa kwa kuzingatia miongozo na taratibu zilizowekwa ili kuhakikisha maji yanayohifadhiwa yanakidhi mahitaji ya uzalishaji wa umeme wa maji pamoja na matumizi mengine ya rasilimali za maji.
- Katika kipindi cha kiangazi, watumiaji wote wa maji wanapaswa kuzingatia masharti na viwango vya uchukuaji wa maji vilivyobainishwa katika vibali vyao vya matumizi ya maji, ili kuhakikisha matumizi endelevu na usimamizi bora wa rasilimali za maji zilizopo.

